



MANCHESTER SCHOOL DISTRICT  
SCHOOL ADMINISTRATIVE UNIT NO. 37  
195 McGregor Street, Suite 201  
Manchester, NH 03102  
Telephone: 603.624.6300 • Fax: 603.624.6337

---

David M. Ryan  
Assistant Superintendent  
Curriculum & Instruction

Christine D. Martin, Ed.D.  
Assistant Superintendent  
Elementary Education

Bolgen Vargas, Ed.D.  
Superintendent of Schools

Karen DeFrancis  
Business Administrator

Pamela D. Hogan  
Director of Human Resources

16 Februari, 2017

Wapendwa wazazi na walezi:

Kama mjuavyo, jiji letu limekuwa likikabiliwa na janga la matumizi mabaya ya opioid (dawa za kutuliza maumivu). Maisha ya wanafunzi wetu wengi yameathiriwa na hatari za matumizi ya mihadarati na kutawaliwa, moja kwa moja au kwa namna nyingine. Mojawapo ya vizio bora kwa tishio hili ni elimu na ufahamu.

Kwa bahati nzuri, tuna washiriki wa kutegemewa wa kutusaidia katika kupambana na janga hili. Utawala wa Kupambana na Mihadarati umeijumuisha Manchester iwe sehemu ya kampeni yake ya nchi nzima, inayoitwa Mkakati wa DEA 360, inayotegemea watekelezaji sheria na shirikiano za jamii kupambana na janga la fentanyl, heroini na opioid ya matibabu. DEA 360 ni mkakati mpana wa kutekeleza sheria na uziujaji wa kuyasaidia majiji katika kupambana na janga la matumizi mabaya ya maagizo ya daktari na heroini na uhalifu wenye vita unaohusika. Maelezo mengi zaidi yanaweza kupatikana kwenye <https://www.dea.gov/prevention/360-strategy/360-strategy.shtml>.

Miongoni mwa mipango ya mkakati ni Mkutano wa Vijana wa New Hampshire unaohusu Ufahamu wa Opioid, ulioandaaliwa na Mkakati wa DEA 360 na Mark Wahlberg Youth Foundation. Tukio hili ni **la siku nusu** linalokusudiwa kuwaelimisha wanafunzi wa shule za msingi na shule za upili kuhusu hatari za kutawaliwa na opioid huku likikuza manufaa ya kuwa na afya nzuri.

Shule zetu zimealikwa kushiriki kwa kuleta wanafunzi wetu mkutanoni katika Uwanja wa SNHU tarehe 7 Machi. Mkutano utaonyesha maonyesho ya "If Only," filamu fupi iliyotayarishwa pamoja na James Wahlberg inayozungumzia madhara ya matumizi mabaya na kutawaliwa na opioid. Mzungumzaji wa wazo kuu Jeff Allison, mzaliwa wa New England na aliyekuwa mtupaji mtaalam wa besiboli, atashiriki hadithi yake binafsi ya kutawaliwa na kupata nafuu tena. Wanafunzi pia watawasikiza wasemaji wengine wakiongea kuhusu hadithi zao binafsi au za familia na wajadiliane kuhusu jukumu muhimu la vijana katika kuzuia matumizi mabaya ya opioid.

Maelezo mengi zaidi kuhusu Mkutano wa Vijana wa New Hampshire unaohusu Ufahamu wa Opioid yanaweza kupatikana kwenye [www.drugfreeisuptomenh.org](http://www.drugfreeisuptomenh.org).

Hakuna gharama ya kuhudhuria tukio hili. Wanafunzi watapata vyakula vya mchana vilivyobebwa kwenye mifuko au wakipenda, majukwaa ya vyakula uwanjani yatafunguliwa kwa wale wanaotaka kununua chakula cha mchana katika tukio. **(WA)MWANAFUNZI ANAWEZA KUAMUA KUTOSHIRIKI KATIKA TUKIO HILI. IKIWA HUTAKI (WA)MWANAFUNZI WAKO AHUDHURIE TUKIO HILI, TAFADHALI JAZA MISTARI ILIYOKO HAPU CHINI NA WARUDISHE BARUA HII KWA OFISI KUU SHULENI KABLA YA ALHAMISI, 23 FEBRUARI.**

---

Bolgen Vargas, Ed.D. Superintendent	John Vaccarezza Principal, CHS	Arthur Adamakos Principal, MHS	Richard Dichard Principal, WHS	Karen Machado Principal, MSTHS
--	-----------------------------------	-----------------------------------	-----------------------------------	-----------------------------------

---

\_\_\_\_ Simruhusu mtoto wangu, \_\_\_\_\_, ahudhurie Mkutano wa Vijana wa New Hampshire unaohusu Ufahamu wa Opioid tarehe 7 Machi.

Saini ya Mzazi/Mlezi: \_\_\_\_\_